



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA  
SUMBAWANGA



Kumb Na. SMC/C.20/11/06

25.04.2023

### TANGAZO LA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga imepokea kibali cha Ajira mpya kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye **kumb. Na. FA.97/228/01" TEMP"06** cha tarehe 06.04.2023. Kufuata idhini hiyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kutuma maombi ya nafasi hizo kwa kuzingatia sifa, vigezo, na maelekezo yaliyo katika tangazo hili.

#### 1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (VE III) – Nafasi 20

##### 1.1 Kazi Na Majukumu.

- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mpango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa rai ana mali zao
- Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote za nyaraka za Kijiji.
- Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji
- Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kupokea na kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- Kazi nyingine atakazopangiwa na mwajiri.

##### 1.2 Sifa za Mwombaji.

- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au sita pia awe amehitimu mafunzo ya **Cheti/Astahada** katika moja ya fani, zifuatazo: - **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa** kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(ANGALIZO: Astashahada/Cheti kiwe na ngazi ya NTA – LEVEL 5)

1.3 Ngazi ya Mshahara ni TGS B.

2.MTENDAJI WA MTA A DARAJA LA III (ME III) – Nafasi 25

2.1 Kazi na Majukumu

- Mratibu na Mtekelezaji wa sera na sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya Maendeleo katika Mtaa.
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umasikini katika Mtaa.
- Kusimamia Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu zawalipa kodi wote.
- Kuandaa na kutunza rejesta ya wafanyakazi wote wa Mtaa.
- Kusimamia Utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo ndogo za mitaa.

2.2 Sifa za Mwombaji.

- I. Cheti cha Kidato cha IV au VI
- II. Aliyehitimu mafunzo ya **Astahada/Cheti** katika moja ya fani zifuatazo:  
**Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi** ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.
- III. Awe hajawahi kuajiriwa Serikalini.

(ANGALIZO: Astashahada/Cheti kiwe na ngazi ya NTA – LEVEL 5)

2.3 Ngazi ya Mshahara ni TGS B.

3. MAMBO YA KUZINGATIWA KWA WAOMBAJI.

1. Muombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.
2. Awe mwenye umri kati ya **18 - 45**
3. Barua za muombaji ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa na Picha mbili (2) za rangi (Passport size) za hivi karibuni.
4. Maombi ya kazi yaambatanishwe na nakala ya Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
5. Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo binafsi ya muombaji (CV)


6. Testimonials "Provisional Result" Statement of Result" hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and Form VI Results Slips) **HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (**NECTA**)

Namna ya Kuwasilisha maombi: -

Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na iambatanishwe na passport size mbili (2).  
Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **08/05/2023** saa **9:30** Alasiri

Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo: -

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga,  
S.L.P 187,  
**SUMBAWANGA.**



Jacob J. Mtalitinya  
**MKURUGENZI MANISPAA  
SUMBAWANGA.**

**MKURUGENZI MANISPAA  
MANISPAA YA SUMBAWANGA**